



# Wavuvi waomba mashine kuanika, kukaushia dagaa

Na Restuta Damian,  
BUKOKA

**B**AADHI ya wavuvi wa mwalo wa dagaa Nyamkazi uliopo Kata ya Miembeni, Manispaa ya Bukoba, mkoani Kagera wameiomba serikali kuwasaidia upatikanaji wa mashine za kuanika na kukaushia dagaa hususani katika msimu wa masika ili kudhibiti hasara.

Wakizungumza na Nipashe jana katika mwalo huo, wavuvi hao pamoja na wachuuzi wa dagaa walisema biashara hiyo inakuwa ngumu kipindi cha mvua kutokana na kutegemea mionzi ya jua kukausha

dagaa wao baada ya kutoka ziwani na kuomba msaada wa mashine za kukaushia.

“Hali hii inafanya kushuka kwa mapato ya wavuvi kutokana na dagaa kuharibika wakati mwingine kuuzwa kwa bei ya hasara ili waishe, lakini tungelikuwa na mashine wangekaushwa na kuuzwa kwa bei rafiki na kufanya biashara hii kuongeza pato la taifa,” alisema Shaidu Mshamba, mvuvi.

Aneth Anatory, mnunuzi wa dagaa mwalo wa Nyamkazi alisema, upatikanaji wa dagaa kwa sasa ni mzuri, lakini tatizo kubwa ni jinsi ya kukausha dagaa hao kutokana na kukosa

sehemu ya uhakika zaidi ya kutegemea jua ambalo kwa kipindi cha masika linawaka kwa shida. “Zikiwapo mashine hizo hata kwa kuzikodi au kukopeshwa itatubidi tugharamikie maana unakuta mtu amenunua ndoo saba hadi kumi ambazo kwa ndoo moja inauzwa Sh. 25,000 katika msimu wa kiangazi, lakini kwa masika ndoo hiyo hiyo inakuwa Sh.10,000, lakini anaingia hasara kubwa pale jua lisipowaka,” alisisitiza Aneth.

Mwenyekiti wa ulinzi na usimamizi rasimili za wavuvi mwalo wa Nyamkazi alisema, tayari wamepokea ombi hilo kutoka kwa wavuvi na wachu-

uzi wa dagaa na limefikishwa serikalini kwa utekelezaji.

Ofisa Uvuvi Mkoa wa Kagera, Ebrahim Mkama, alisema, ili kusaidia wavuvi hao ni kuwapa elimu ya ushirikiano baina yao na taasisi za kifedha mkoani humo ili wapatiwe mikopo itakayowawezesha kununua mashine hizo na kuzimiliki wenyewe.

Alisema zipo kampuni zinazotengeneza mashine ikiwamo (SIDO) zenye uwezo wa mitambo hiyo na kupeleka kwenye maeneo yao ya kuanika dagaa, ni suala la wao kununua na serikali imewapatia tayari maeneo ya kuanika dagaa wao.



(CCM), aliyetaka kujua ni lini serikali itakarabati shule za msingi kongwe

HABARI LEO UK 18.

## \* Mashamba darasa 100 ya malisho kuanzishwa

**K**ATIKA mwaka wa fedha 2022/23, serikali imeanzisha mashamba darasa 100 ya malisho katika halmashauri 44 zikiwamo zinazopakana na Bonde la Ihefu na Mto Kilombero.

Mashamba darasa hayo yameanzishwa ili wafugaji wajifunze kuzalisha malisho na hivyo kutulia katika maeneo yao ya ufugaji.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, David Silinde alitoa kauli hiyo wakati akijibu swali la Mbunge wa Donge, Mohammed Jumah Soud (CCM).

Katika swali lake, Soud alitaka kujua kuna mkakati gani wa kudhibiti mifugo katika bonde la Ihefu na Mto Kilombero.

Silinde alijibu, Oktoba, 2022 serikali kupitia Kamati ya Mawaziri wanane wa Kisekta inayoshughulikia migogoro ya ardhi katika vijiji 975 nchini, ilitoa tamko kuhusu utatuzi wa mgogoro wa mpaka kati ya Hifadhi ya Taifa Ruaha na baadhi ya vijiji vya wilaya za Mbarali na Chunya.

"Ili kudhibiti mifugo katika bonde la Ihefu na Mto Kilombero, jumla ya vijiji 16 vimeandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji na kutenga maeneo kwa ajili ya malisho ili kuwezesha ufugaji katika maeneo hayo," alieleza.

Alisema ili kudhibiti mifugo kutoka katika maeneo mengine kwenda kwenye bonde la Mto Kilombero kutafuta malisho na maji, katika mwaka 2022/23, serikali inajenga mabwawa ya maji kwa ajili ya mifugo katika Halmashauri za Morogoro DC Kijiji cha Kongwa na Kibaha DC Kijiji cha Viyenze.

\* V

R

E

ku: za wa ish zar mi ina ma

mw 202 za k zim kug wal

mo, (pic hiyo la M Vijji Nde

alita kali ruzi dav

'V

V

vyuc vinal K wa A ya M ya W irikia Sterg la M